MBOLEA BORA KWA KILIMO ENDELEVU

# Mbolea YETU

Tanzania ISSN 2799-2039 Toleo Na. 07 - Machi 2024

**Toleo Maalum**




**3@3**

# Mageuzi Makubwa tasnia ya MBOLEA



## Miaka 3 ya Rais Samia Ofisini

UJUMBE WA
**MKURUGENZI MTENDAJI**



*Joel Laurent*
*Mkurugenzi Mtendaji*

# Maono ya Rais Samia yameleta mageuzi sekta ya kilimo

Ni jambo la kushukuru kwamba uongozi wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan umeleta mageuzi makubwa katika sekta ya kilimo, ambayo ndiyo mhimili wa uchumi wa nchi yetu.

Maono na dhamira ya Rais kuhusu uimarishaji wa kilimo yameshuhudia ongezeko la uzalishaji wa mazao mbalimbali ya chakula na biashara, na hivyo kuisadia nchi yetu kuwa na uhakika wa usalama wa chakula.

Uzalishaji katika sekta ya kilimo umeongezeka kutokana na vitendo thabiti kuhakikisha kwamba nchi yetu inajitegemea kwa chakula na kuzalisha ziada kwa ajili ya kupata fedha za kigeni zitusaidie katika maendeleo ya taifa letu.

Pamoja na uzalishaji chakula, pia tunahitaji malighafi za kutosha ili kulisha viwanda vyetu vya ndani.

Ni kutokana na azma hii ya Serikali ya Awamu ya Sita katika uongozi wa miaka mitatu wa Rais Samia tumeshuhudia mafanikio makubwa ya kukua kwa tasnia ya mbolea, tasnia ambayo kwa miaka ya nyuma haikupewa kipaumbele cha kutosha ili iweze kuchangia uzalishaji mazao kwa wingi.

Katika kipindi cha mwaka 2020/21 hadi 2023/24 biashara ya mbolea imeshamiri, hasa kutokana na uongezekaji wa upatikanaji wake kutoka tani 582,351 mwaka 2020/2021 hadi kufikia tani 1,115,841 mwaka 2023/2024.

Ongezeko hili la upatikanaji wa mbolea limechochewa na serikali kuweka mazingira wezeshi ya biashara ya pembejeo hiyo muhimu katika kilimo.

Ni jambo la faraja kwamba ongezeko hili la upatikanaji wa mbolea pia limechochea matumizi yake kutoka tani 475,000 mwaka 2020/2021 hadi tani 848,000 mwaka 2023/24.

Hizi ni juhudi za makusudi za serikali za kuweka sera wezeshi, hasa Mpango wa Mbolea ya Ruzuku, ambao umemwezesha mkulima kupata mbolea kwa bei nafuu.

Serikali pia imeweka mazingira wezeshi ya uingizaji na usambazaji wa mbolea nchini pamoja na kuweka bei elekezi inayompatia mfanyabiashara faida na pia kumpa unafuu mkulima.

Katika kipindi hiki cha miaka mitatu tumeshuhudia kampeni ya kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi sahihi ya mbolea kwa kilimo endelevu na chenye tija.

Pia serikali ilianzisha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo kusaidia kupunguza gharama za mbolea na kuhamasisha uwekezaji katika ujenzi wa viwanda vya mbolea vya ndani na kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima.

Lengo la Mpango wa Ruzuku kuanzia mwaka 2022/23 ambapo serikali ilitenga shilingi bilioni 150 ni kuwapunguzia wakulima makali ya bei.

Mantiki ya ruzuku ya mbolea kwa nchi kama yetu inayoshuhudia kasi ya ongezeko la idadi ya watu ni kuimarisha usalama wa chakula na kuongeza malighafi viwandani.

Hayo yote ni mafanikio chini ya uongozi wa Rais Samia ambaye amedhamiria kuleta mageuzi ya kuimarisha sekta ya kilimo.

Kwa hakika, haya ni mageuzi ya kutukuka, hasa katika taifa ambalo zaidi ya asilimia 65 ya wananchi wake vijijini wanategemea kilimo kwa ustawi wa maisha yao.

Kama alivyosema mvumbuzi Mwingereza, Francis Drake, alipoizunguka dunia miaka 428 iliyopita, mambo makubwa yana mwanzo mdogo. Kwa Tanzania tumeanza polepole kubadili kilimo chetu, na hatima yake ni matarajio ya mafanikio makubwa kwa miaka ya usoni.

## BODI YA UHARIRI

*JOEL LAURENT* - *MWENYEKITI*

*MATILDA KASANGA* - *KATIBU*

*DANIEL MAARIFA* - *MJUMBE*

*RAYMOND KONGA* - *MJUMBE*

*AZIZI MTAMBO* - *MJUMBE*

*SALEHE KEJO* - *MJUMBE*

*THERESIA SIRIWA* - *MJUMBE*

*NURU MWASAMPETA* - *MJUMBE*

*ALPHA NUHU* - *MJUMBE*



## Miaka 3 ya Rais Samia Ofisini

# TAHARIRI

## Miaka mitatu ya Rais Samia tumeshuhudia mapinduzi sekta ya kilimo

KWA mtazamo wa kawaida wa mwanadamu, miaka mitatu katika uhai wa taifa si kipindi kirefu kufanyika mambo mengi makubwa ya kujivunia.

Lakini kwa kipindi hicho cha miaka mitatu, Serikali ya Awamu ya Sita ya Rais Samia Suluhu Hassan imeleta mageuzi makubwa kwa kila sekta kuonyesha kwamba inataka mapinduzi ya kiuchumi kwa Tanzania katika karne hii ya 21.

Dhamira hiyo ya serikali imejionyesha dhahiri katika sekta kuu ya kilimo. Moja ya mageuzi yanayoonekana bayana katika sekta hiyo ni kuongezeka kwa uwekezaji wa raslimali fedha katika bajeti ya Wizara ya Kilimo ambayo imeongezeka kutoka shilingi bilioni 294 mwaka 2021/22 hadi kufikia shilingi bilioni 971 mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 230.

Tangu enzi za ukoloni zaidi ya miongo sita iliyopita, sekta ya kilimo imeendelea kuwa nguzo kubwa ya uchumi wa Tanzania, na itaendelea kuwa hivyo kwa miongo mingi ijayo kwa sababu ndiyo sekta inayoajiri asilimia 75 ya mamilioni ya Watanzania wote.

Kwanini ni muhimu kuwekeza katika sekta ya kilimo? Hili ndilo swali ambalo wataalam wa uchumi wamekuwa wakijiuliza mara kwa mara. Jibu pengine ni rahisi: Hii ndiyo sekta inayobeba usalama wa chakula kwa idadi kubwa ya watu wanaongezeka kwa kasi kila mwaka; hii pia ndiyo sekta inayozalisha malighafi zinazohitajika viwandani.

Kilimo pia ndiyo sekta ambayo ni chanzo cha mazao ya kibiashara yanayozalishwa na kusafirishwa nchi za nje kupata fedha za kigeni na kuagiza bidhaa mbalimbali zinazohitajika kwa maendeleo ya taifa.

Wakati watu wengi wanapojihusisha na kilimo, uzalishaji unakuwa ni nguzo kuu ya pato la taifa kwa sababu sekta hiyo inakuwa msingi wa kodi na chanzo cha akiba ya fedha za matumizi katika miradi ya maendeleo.

Ni lazima ieleweke wazi kwamba uchumi wa nchi zinazoendelea kama Tanzania unategemea zaidi uzalishaji wa chakula. Ukweli huu kwa Watanzania umekuwa ukirudiwa na marais wa awamu zote tangu kupatikana kwa uhuru kwenye miaka ya mwanzo ya 1960.

Watanzania waliobahatika kuishi katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru 1961-2021 wameshuhudia kaulimbiu nyingi kuhusu kilimo: Siasa ni Kilimo, Kilimo cha Kufa na Kupona, Kilimo ni Uhai na Kilimo Kwanza.

Kaulimbiu hizi zote zililenga uwekezaji katika kilimo ili kuchochea ukuaji wa uchumi kwa ujumla wa taifa hili kubwa la Afrika Mashariki.

Kuthibitisha kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania katika kipindi cha mwaka 2019 hadi 2022 sekta hiyo imekuwa ikichangia kati ya asilimia 26.1 hadi 26.9 ya pato la taifa. Licha ya mchango wa moja kwa moja kwenye pato la taifa, pia sekta hiyo imechochea ukuaji wa sekta nyingine kwa kuzalisha asilimia 65 ya malighafi za viwanda vya ndani na kuchangia kati ya asilimia 114 hadi 126 ya utoshelevu wa chakula nchini.

Hakika, katika mazingira ambayo kilimo ndiyo sekta kuu ya uchumi, maendeleo ya uchumi ya taifa lolote yanategemea zaidi mafanikio ya sekta hiyo.

Ndiyo maana kwa kuzingatia ukweli huo, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imepania kuleta mapinduzi ya kilimo nchini. Wizara ya Kilimo ikiongozwa na Waziri Hussein Bashe imeweka Agenda 10/30 Kilimo ni Biashara yenye lengo la kuhakikisha kuwa sekta ya kilimo inafikia ukuaji wa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030.

## YALIYOMO



Mazingira wezeshi ya uongozi wa Samia yalivyochochea ukuaji tasnia ya mbolea **Uk > 6**



*Kiwanda cha mbolea Minjingu kuongeza uzalishaji Mei 2024* ***Uk > 10***



*Mchango wa tasnia ya mbolea katika ukuaji wa uchumi* ***Uk > 12***



*TFRA yatanua wigo kwa kuwavuta wawekezaji tasnia ya mbolea* ***Uk > 13***



*Rais Samia afurahishwa na ongezeko matumzi ya mbolea* ***Uk > 14***

# Biashara ya mbolea yashamiri nchini




*Waziri wa Kilimo, Hussen Bashe (Kushoto) na Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde wakiwa wamenyanyua mfuko wa mbolea ya Ruzuku wa kilo hamsini (50) wakati wa hafla ya uzinduzi wa usajili wa wakulima katika msimu wa kilimo kwa mwaka 2022/2023.*

Na **MWANDISHI WETU**

**Biashara ya mbolea** nchini imeimarika zaidi katika kipindi cha miaka mitatu kutoka tani 582,351 mwaka 2020/21 hadi kufikia tani 1,115,841 mwaka 2023/24, kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent.

Laurent amesema mazingira wezeshi ndiyo kichocheo kikubwa cha kuongezeka kwa upatikanaji mbolea nchini katika kipindi hicho cha miaka mitatu .

Kwa kipindi hicho cha miaka mitatu 2020/21 hadi 2023/24 TFRA ilifanikiwa kuingiza mbolea aina ya Urea, DAP, SA, NPK, MAP, MOP,SOP TSP na nyinginezo.

Kwa mujibu wa takwimu hizo za TFRA, katika msimu wa 2022/23 mbolea zilizouzwa ni jumla ya tani 580,629 ambazo kati ya hizo tani 386,262 zenye thamani ya Shilingi 876,633,529,270/- ziliuzwa katika Mpango wa Ruzuku.

Katika kiasi hicho cha fedha, ruzuku ya serikali ni Shilingi 370,898,554,271/- na fedha ya wakulima ni Shilingi 505,734,675,000/-.

Tasnia ya mbolea nchini bado kwa asilimia 90 inategemea mbolea zinazoagizwa kutoka nje ya nchi, jambo ambalo wataalam katika tasnia hiyo wanasema huathiri upatikanaji wake na wakati mwingine kusababisha kupanda kwa bei ya pembejeo hizo kwa matumizi ya wakulima.

Hali hiyo kwa ujumla wake husababisha matumizi madogo ya mbolea na kuathiri uzalishaji na tija wa mazao mbalimbali.

Kupanda kwa bei za mbolea katika soko la dunia na athari zake hapa nchini ndicho kiini kilichoisukuma serikali kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Ruzuku ya Mbolea ili kuwapunguzia wakulima gharama na kuongeza tija ya uzalishaji.

Kupanda huko kwa bei ya mbolea kulisababishwa na athari za UVIKO-19 pamoja na mgogoro wa Urusi na Ukraine, hali ambayo ilichangia kushuka kwa matumizi ya mbolea, tija kwa mazao mbalimbali.



## Miaka 3 ya Rais Samia Ofisini



*KUSHOTO: Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Anthony Diallo (wa tatu kushoto) akizungumza na mawakala (picha ya kulia) wa mbolea wa Nyanda za Juu Kusini katika kikao kilichofanyika Jijini Mbeya Oktoba 18, 2023 wakati wa ziara ya wajumbe wa Bodi iliyolenga kusikiliza changamoto za mawakala wa mbolea na kuzitatua.*



*Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti wa Mamlaka, Happines Mbelle (katikati) akiwa katika picha na wataalam wa maabara ya mbolea mara baada ya kukamilika kwa jengo na kusimika baadhi ya mitambo na vifaa vya maabara hiyo.*



*Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti wa Mamlaka, Happiness Mbelle akiwa katika picha na wataalam wa maabara katika lango la kuingilia kwenye maabara ya mbolea hivi karibuni.*





# Mazingira wezeshi ya uongozi wa Samia yalivyochochea ukuaji tasnia ya mbolea



*Waziri wa Kilimo Mh. Hussein Bashe akiwasilisha Bungeni Hotuba ya makadirio na matumizi ya wizara ya Kilimo kwa Mwaka 2022-2023 ambayo bajeti ya Wizara ya kilimo iliongezwa na kutenga kiasi cha shilingi bilioni 150 ili kitumike kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima.*




*Mwonekano wa jengo la maabara ya mbolea iliyojengwa kwa lengo la kuboresha huduma za udhibiti unaosimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa mbolea Tanzania (TFRA) iliyojikita katika kuchambua ubora wa mbolea zinazozalishwa na kuingizwa nchini kutoka nje ya nchi.*

Na **MWANDISHI WETU**

**UTASHI wa kisiasa** uliojenga mazingira wezeshi ni nyenzo muhimu iliyosaidia kasi ya ukuaji wa tasnia ya mbolea nchini katika kipindi cha miaka mitatu cha uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alipoingia madarakani mapema 2021, Rais Samia na serikali yake ulibuniwa mpango kabambe wa kitaifa wa kutoa ruzuku ya mbolea kuimarisha sekta ya kilimo iweze kutoa mchango mkubwa katika uchumi wa taifa.

Mpango huo wa Mbolea ya Ruzuku sasa umeleta hamasa kubwa miongoni mwa wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali, kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA).

Ni katika kipindi hiki cha miaka mitatu cha uongozi wa Rais Samia kwamba Tanzania imeshuhudia kasi ya ujenzi wa viwanda vya mbolea na visaidizi vyake kutoka 12 hadi 15, na hivyo kuchochea ongezeko la upatikanaji wa mbolea nchini ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

## ONGEZEKO BAJETI YA KILIMO

Hali kadhalika, ni katika kipindi hiki cha miaka mitatu chini ya uongozi wa Rais Samia bajeti ya Wizara ya Kilimo imepanda kutoka shilingi 751.123,280,000 mwaka 2022/2023 hadi shilingi 970,785,619,000 mwaka 2023/2024.

Bajeti hiyo ni kuonyesha msukumo mkubwa uliowekwa na serikali katika kuimarisha sekta ya kilimo ambayo inaajiri asilimia 75 ya Watanzania, hasa maeneo ya vijijini, anaeleza Mkurugenzi wa TFRA, Joel Laurent.

Mafanikio haya yakijumuishwa na ujenzi wa maabara ya kisasa ya uchambuzi wa mbolea jijini Dar es Salaam, ni jitihada za makusudi za serikali za kutatua changamoto mbalimbali kwenye tasnia ya mbolea na kutengeneza mazingira wezeshi kwa wawekezaji.

*Inaendelea Uk > 7*



## Miaka 3 ya Rais Samia Ofisini

# Mazingira wezeshi ya uongozi




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akikata utepe kuashiria uzinduzi wa utekelezaji wa Mpango wa Mbolea za ruzuku kwa wakulima wakati wa kilele cha sherehe za wakulima maarufu kama nanenane zilizofanyika tarehe 8/8/2022 Jijini Mbeya*

*< Inatokaa Uk 6*

Louis Kasera, Kaimu Mkurugenzi Uzalishaji wa Ndani na Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), anakiri kwamba serikali imefanya kazi kubwa kuweka mazingira wezeshi katika kila sekta ya kiuchumi, ikiwemo tasnia ya mbolea, ili kuwavuta wawekezaji wa nje na wa ndani kuchangamkia fursa zilizopo katika tasnia ya mbolea.

Kasera anaeleza kwamba moja ya kichocheo kikubwa katika tasnia ya mbolea ni upatikanaji wa malighafi za viwanda kwa ajili ya uzalishaji wa mbolea. Malighafi hizo ni pamoja na madini ya fosfeti, gesi asilia tani za ujazo trilioni 57, uwepo wa makaa ya mawe ya kutosha, madini ya chokaa na madini mengine yanayohitajika ambayo yametawanyika katika maeneo mbalimbali nchini.

Rais Samia na viongozi waandamizi katika Wizara ya Kilimo na taasisi zake wanaamini kwamba Tanzania ni nchi iliyojaliwa fursa za uwekezaji katika viwanda vya mbolea kwa sababu ni taifa lililozungukwa na soko kubwa la nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara lenye idadi ya watu zaidi milioni 600.

Asilimia 90 ya mbolea zinazotumika Tanzania zinaagizwa kutoka nje wakati kiasi kilichobaki cha asilimia 10 ndicho kinachozalishwa na viwanda 15 vilivyopo nchini kwa sasa, hii ni kwa mujibu wa takwimu za TFRA.

Azma ya serikali ni kuona kwamba Tanzania inajenga mazingira ya kujitosheleza kwa pembejeo kama mbolea ili kuepuka uagizaji kutoka nje – hasa kutokana na gharama za matumizi ya fedha za kigeni.

Kiwanda cha Minjingu ni kiwanda kikubwa ambapo kinazalisha visaidizi vya mbolea kwa asilimia 80 ya visaidizi vya

*Inaendelea Uk > 8*





Miaka 3 ya Rais Samia Ofisini

# Mazingira wezeshi ya uongozi

< Inatokaa Uk 7

mbolea. Viwanda vingine vinavyozalisha visaidizi vya mbolea ni ABM Equipment kilichopo Tanga na Dodoma Cement cha jiji la Dodoma. Viwanda vingine ni Kahela Traders, Keen Feeders Co. Limited, Sianga Agro Trade Company, Mtali Agrotraders and Amka Feeder's, ambavyo vyote hutengeneza mbolea za majimaji.

### FURSA ZA UWEKEZAJI TASNIA YA MBOLEA

Kwa kuwa mbolea zinazozalishwa nchini hazikidhi mahitaji, Serikali ya Awamu ya Sita imelazimika kubeba jukumu la kuwavuta wawekezaji wamiminike nchini ili kuwekeza kwenye viwanda vya mbolea.

Fursa za uwekezaji zilizopo kwenye tasnia ya mbolea ni pamoja na utashi wa kisiasa na mazingira wezeshi, uwepo wa soko la ndani na nje. Bila ya kuwepo kwa utashi wa kisiasa ni vigumu kwa nchi yoyote duniani inayoweza kufikia malengo 17 ya maendeleo endelevu.

Kwa Tanzania, inayojivunia eneo lake la kijiografia, lipo soko kubwa la mbolea kwenye nchi jirani za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Umoja wa Maendeleo wa nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

### MIUNDOMBINU THABITI SEKTA YA UCHUKUZI

Hivi sasa Tanzania inajivunia kuwepo kwa ujenzi wa miundombinu ya kisasa ya barabara na reli kwa ilii kuimarisha sekta ya uchukuzi. Karibu asilimia 70 na zaidi ya Tanzania sasa inapitika kwa barabara za lami, ukiacha ujenzi wa reli ya kisasa inayoendelea kujengwa kutoka jiji la biashara la Dar es Salaam kwenda nchi jirani za Afrika Mashariki kama vile Rwanda na Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo.

### USALAMA WA CHAKULA

Uamuzi wa serikali ya Tanzania kuweka msukumo mkubwa katika tasnia ya mbolea ni kuimarisha usalama wa chakula kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu la asilimia 4.8 kila mwaka (sasa Tanzania ina watu milioni 63, kwa mujibu wa sensa ya 2022) na pia kuongeza malighafi viwandani.

Katika miaka mitatu ya uongozi wake, Rais Samia amekuwa akiwahimiza watendaji wa ngazi zote kusimamia kikamilifu mageuzi yanayofanyika katika sekta ya kilimo ili sekta hiyo itoe mchango wake kwa uchumi wa taifa.

Rais amekuwa akisisitiza kwamba maamuzi ya serikali kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima ni kuwawezesha kutumia fursa hiyo kuzalisha kibiashara ili kupata chakula cha kutosha pamoja na ziada ya kuuzwa nje ya nchi na kuingiza fedha za kigeni.

### KUANZISHWA MFUKO WA PEMBEJEO

Mama Samia kila wakati amekuwa akisisitiza kwamba ongezeko la uzalishaji mashambani litaifanya serikali kuanzisha mfuko wa pembejeo utakaotumika wakati wa dharura, hasa kunapotokea kupanda kwa bei za pembejeo za kilimo.

Mipango mahsusi ya serikali ya kuongeza uzalishaji wa mbolea nchini ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda cha kisasa cha Itracom Fertilizer Limited kilichopo Dodoma na upanuzi wa kiwanda cha Minjingu mkoani Manyara, ambavyo vyote vitapunguza adha wanayopata wakulima wa kununua mbolea kwa bei kubwa.

Inaendelea Uk > 9



*Mtaalam wa mfumo wa kidigitali wa mbolea za ruzuku Mahamud Shoo (kulia) akiwaelekeza viongozi wa Kijiji cha kata ya Ndagha Tukuyu namna ya kuwasajili wakulima katika vitabu vya ruzuku ili kuwawezesha kuingia katika mfumo wa kidijitali wa uuzaji wa mbolea hizo mapema Agosti 2022 ulipozinduliwa mpango huo*



## Miaka 3 ya Rais Samia Ofisini

# Mazingira wezeshi ya uongozi

*< Inatokaa Uk 8*

Miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia imeshuhudia serikali yake ikijitahidi kuvijengea uwezo viwanda vya mbolea vya ndani na kumjengea uwezo mwekezaji mkubwa wa kiwanda cha mbolea cha Minjingu ili aweze kupata mikopo itakayomsaidia kuendeleza kiwanda hicho ili kuongeza uzalishaji.

Hakuna ubishi kwa miongo mingi ijayo, kilimo kitaendelea kuwa ni uti wa mgongo wa Tanzania kutokana na ukweli kwamba sekta hiyo ndiyo mwajiri mkubwa wa asilimia 75 ya Watanzania wote.

Ndiyo maana tangu Tanzania Bara ipate uhuru wake kutoka Waingereza zaidi ya miaka 60 iliyopita serikali za awamu zote zimekuwa zikitilia mkazo sekta hiyo.

Kampeni inayoendelea nchini kuhusu matumizi ya mbolea kwenye kilimo imehusisha wadau wengi kuanzia wizara mama ya Kilimo, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania, sekretarieti za mikoa, mamlaka ya serikali za mitaa, waingizaji/wazalishaji wa mbolea, mawakala wa mbolea na taasisi za fedha.

Wadau hawa wamehusishwa ili kuhakikisha kwamba kampeni hii ya matumizi ya mbolea katika kilimo haikwami mahali popote. Nia ni kuhakikisha mbolea inamfikia mkulima kwa njia rahisi na kwa bei iliyopangwa na serikali badala ya kupitia njia zisizo halali kama vile ulanguzi wa bidhaa hiyo.

### WAZIRI BASHE NA KILIMO CHA KISASA

Hussein Mohamed Bashe, Waziri wa Kilimo amekuwa ni mhimili mkubwa wa kusimamia kikamilifu suala la matumizi ya mbolea nchini. Zipo taarifa za kutia moyo kwamba katika mikoa mingi nchini matumizi ya mbolea sasa yamezaa matunda kwa kuchochea ongezeko la uzalishaji.

Miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia imeshuhudia ongezeko la matumizi ya mbolea katika kilimo na kuwapa matumaini wakulima ya kubadilika kwa hali zao za maisha siyo tu kiuchumi bali pia kujitosheleza kwa chakula na kuwa ziada ya kuuza. Kwa miongo kadhaa baada ya uhuru, baadhi ya wasomi walikuwa wakikiona kilimo kama ni adhabu au mateso kwa sababu kilikuwa kikionekana hakina tija kwa wakulima.

### WASOMI WAKIMBILIA KILIMO

Kwa Tanzania ya leo, vijana wengi wasomi wameanza kukimbilia kilimo kama chanzo cha asali na maziwa. Katika dunia hii ya ukosefu wa ajira, vijana wasomi sasa wameanza kugeuka wakulima hodari wa mazao mbalimbali ya biashara na chakula.

Msukumo wa Serikali ya Awamu ya Sita kuhusu tasnia ya mbolea umesaidia kuwaelimisha wakulima na wadau mbalimbali kwamba "kilimo kinalipa" kwa watu ambao ni makini katika kujiletea utajiri.

Hamasa ya Rais Samia kuhusu ujenzi wa viwanda vya mbolea imezaa matokeo chanya ya upatikanaji wa mbolea kwa wakati na kwa bei nafuu, na hivyo kuongeza uzalishaji, usalama wa chakula, kudhibiti mfumuko wa bei za vyakula na kuinua kipato cha mkulima.



*Meneja wa Mamlaka Kanda ya Kaskazini Gothard Liampawe akichukua sampuli ya mbolea kwenye meli iliyokuwa ikishusha mbolea katika bandari ya Dar es Salaam kwa ajili ya kujiridhisha na ubora wake.*



Miaka 3 ya Rais Samia Ofisini



# Kiwanda cha mbolea Minjingu kuongeza uzalishaji Mei 2024

Na **MWANDISHI WETU**

**Kampuni ya Mbolea ya Minjingu Mines & Fertiliser Limited (MMFL)** imejipanga kuongeza uzalishaji kutoka tani 100, 000 zinazozalishwa sasa hadi kufikia tani 250,000 ifikapo mwezi Mei 2024.

Akizungumza na Jarida la Mbolea Yetu linalochapishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Mkurugenzi Mkuu wa MMFL Hans Tosky amesema maandalizi ya kuanza uzalishaji huo yako ukingoni ambapo usimikaji wa mitambo mipya unaendelea ambayo itakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 150, 000 hivyo kuongeza uzalishaji na kuwa jumla ya tani 250,000 ifikapo mwezi Mei 2024.

Kampuni ya Minjingu Mines and Fertilizer Limited ni kampuni ya Kitanzania inayozalisha mbolea kwa kutumia madini adimu ya viwandani ya asili ya Phosphate.

Tosky amesema Madini hayo huchimbwa, huchakatwa na kuchanganywa na virutubisho vingine kwa lengo la kupata lishe kamili ya mimea kulingana na mahitaji na hali halisi ya afya ya udongo.

Virutubisho vinavyoongezewa kwenye Phosphate ya asili huweza kutengeneza mbolea zenye virutubisho muhimu vya upili na vidogo vidogo.

"Kwa sasa kiwanda kina uwezo wa kuzalisha tani 100,000 za aina mbalimbali za mbolea kwa mwaka. Aidha, usimikaji wa mitambo mipya unaendelea ili kuongeza uwezo wa kuzalisha tani 150,000 za ziada kwa mwaka," amesema Tosky. Hivyo basi kuanzia mwezi Mei 2024, MMFL itakuwa na uwezo wa kuzalisha jumla ya Tani 250,000 kwa mwaka, aliongeza Tosky.

Tosky amesema dira ya MMFL ni kuwa mzalishaji na msambazaji wa mbolea zinazohitajika kwa wingi Tanzania na Ukanda wa Afrika Mashriki kwa kutumia madini ya viwandani ya Phosphate yanayolinda bioanuai katika udongo wenye viwango tofauti vya tindikali na alkali.



## Miaka 3 ya Rais Samia Ofisini

### Mbolea za MMFL zilizosajiliwa na kuthibitishwa ubora wa viwango kama jedwali linavyoonesha:

| Na. | Mbolea | Virutubisho | Imesajiliwa | Imethibitishwa | Matumizi |
|---|---|---|---|---|---|
| i. | Nafaka Plus | NPK 09:16:06 + 05%S, 25%CaO, 02%MgO, 01%Zn, 0.01%B | TFRA Cert. No. 0022 | TBS 778/EAS 912 | Kupandia mazao ya Nafaka (Mahindi, Mpunga, Mtama, Ngano, Uwele, Shayiri); Mikunde (Maharage, Kunde, Choroka, Mbaazi); Mboga & Viungo (Kabichi, Bamia, Karoti, Matango, Tangawizi); Mafuta (Alizeti, Ufuta, Karanga) |
| ii. | Top Dressing | NPK 27:10:00 + 15%CaO | TFRA Cert. No. 0277 | TBS 778/EAS 912 | Kukuzia mazao ya Nafaka (Mahindi, Mpunga, Uwele, Ngano, Shayiri); Mboga & Viungo (Kabichi, Bamia, Karoti, Matango, Tangawizi); Mbegu za Mafuta (Karanga, Alizeti, Ufuta); Majani (Tumbaku) |
| iii. | Pamba | NPK 10:10:20 + 4%S, 13%CaO, 01%MgO, 01%Zn, 0.5%B | TFRA Cert. No. 0433 | TBS 778/EAS 912 | Kupandia na Kukuzia Pamba na Mazao mengine yenye uhitaji mkubwa wa kirutubisho cha Potasiamu |
| iv. | Coffee Plus | NPK 20:10:15 + 09%CaO, 0.5%MgO | TFRA Cert. No. 0432 | TBS 778/EAS 912 | Kupandia na Kukuzia Mibuni na Mazao mengine yenye uelekeo wa mahitaji ya virutubisho tajwa |
| v. | Golden Leaf Tobacco | NPK 10:18:24 + 07%S, 04%CaO, 0.4%MgO, 0.12%B | TFRA Cert. No. 0267 | TBS 778/EAS 912 | Kupandia na Kukuzia Tumbaku na Mazao mengine yenye uhitaji mkubwa wa potasiamu. |
| vi. | Golden Chai | NPK 25:05:15 + 03%S, 05%CaO, 0.4%MgO, 0.5%Zn, 0.02%B | TFRA Cert. No. FERT/5278 | TBS 778/EAS 912 | Kupandia na Kukuzia Chai na Mazao mengine yenye uhitaji mkubwa wa kirutubisho cha Potasiamu |
| vii. | Organic Hyper Phosphate | NPK 00:28:00 + 36%CaO, 2.5%MgO | (i) Tan Certificate No. 0020-07-001 (ii) TFRA Cert. No. 0151 | TBS 988 / EAS 904 | Kupandia Mazao ya Miti (Parachichi, Mchikichi, Mibuni, Korosho, Michungwa, Mifenesi); Sukari (Miwa); Matunda (Migomba, Nanasi, Mipapai, Makakara); Nyuzi (Katani, Pamba); Mizizi (Mihogo, Magimbi, Viazi); na Bustani. |



Miaka 3 ya Rais Samia Ofisini

# Mchango wa tasnia ya mbolea katika ukuaji wa uchumi

Na **MWANDISHI WETU**

**Sekta ya Kilimo** ni mhimili wa Uchumi wa Tanzania ambapo inaajiri takribani asilimia 65 ya nguvu kazi ya taifa na inachangia takribani asilimia 24 ya mauzo ya nje. Katika kipindi cha mwaka 2019 hadi 2022 sekta hiyo imekuwa ikichangia kati ya asilimia 26.1 hadi 26.9 ya pato la taifa.

Akizungumzia mchango wa Tasnia ya mbolea katika kipindi cha miaka mitatu ya Dkt. Samia Suluhu Hassan madarakani, Meneja wa Ununuzi wa Mbolea Kwa Pamoja Bi. Elizabeth Bolle anasema kwa muda mrefu Sekta ya Kilimo imekuwa ikitafsiriwa kama uti wa mgongo wa uchumi kwa kuwa pamoja na mchango wake wa moja kwa moja kwenye pato la taifa, vilevile inachochea ukuaji wa sekta nyingine kwa kuzalisha takribani asilimia 65 ya malighafi za viwanda vya ndani na kuchangia kati ya asilimia 114 hadi 126 ya utoshelevu wa chakula nchini.

Bi. Bolle anasema kwenye mazingira ambayo kilimo ndiyo sekta kuu ya uchumi, maendeleo ya uchumi yanategemea zaidi ufanisi katika sekta ya hiyo. Kwa kuzingatia hali hiyo, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeonyesha dhamira ya dhati ya kufanya mapinduzi katika Sekta ya Kilimo kwa kuongeza uwekezaji wa raslimali fedha ambapo bajeti ya Wizara ya Kilimo imeongezeka kutoka takribani bilioni 294 mwaka 2021/22 hadi kufikia takribani bilioni 971 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 230.

"Uwekezaji huo unalenga kuongeza ukuaji wa Sekta ya Kilimo na kuchochea ukuaji wa uchumi kwa ujumla. Katika kutekeleza azma ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuleta mapinduzi ya kilimo nchini, Wizara ya Kilimo chini ya Mhe. Hussein Bashe (Mb), Waziri wa Kilimo imeweka Ajenda 10/30 Kilimo ni Biashara yenye lengo la kuhakikisha kuwa Sekta ya Kilimo inafikia ukuaji wa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030 na kuwezesha shughuli za kilimo kufanyika kibiashara zaidi", anasema Bi Bolle.

Anaongeza kuwa katika kutekeleza Ajenda 10/30 hatua mbalimbali zimechukuliwa ili kuchochea uzalishaji na tija ikiwa ni pamoja na kuongeza matumizi ya pembejeo bora za kilimo hasa mbolea, kuimarisha kilimo cha umwagiliaji, kuimarisha upatikanaji wa huduma za ugani, utafiti, masoko ya mazao na huduma nyingine muhimu.

Kwa mujibu wa Bi. Bolle matumizi ya mbolea katika uzalishaji wa mazao ni muhimu kwa lengo la kurutubisha na kuboresha afya ya udongo ili kuweza kuzalisha mazao kwa wingi.

Anasema matumizi ya mbolea kwa sasa ni ya muhimu zaidi kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kuongezeka kwa idadi ya watu kunahitaji ongezeko la uzalishaji wa chakula kukidhi mahitaji; ukuaji wa miji, miundombinu na huduma nyingine za kijamii unapunguza eneo linalofaa kwa kilimo na hivyo eneo linalobaki linatakiwa kutumika kwa ufanisi kwa kuongeza tija.

Sababu anasema nyingine ni pamoja na hamasa ya utunzaji wa mazingira kwa kuepuka ukataji wa miti kwa ajili ya kuanzisha mashamba mapya na hivyo kulazimu kuongeza uzalishaji katika eneo moja.

Kuongeza tija ya uzalishaji kupitia matumizi sahihi ya mbolea Bi. Bolle anasema kunachangia kuongeza kipato cha mkulima mmoja mmoja, ukuaji wa Sekta ya Kilimo na pato la taifa.



**Mbolea inachochea ukuaji wa sekta nyingine kwa kuzalisha takribani asilimia 65 ya malighafi za viwanda vya ndani na kuchangia kati ya asilimia 114 hadi 126 ya utoshelevu wa chakula nchini.**

Kwa kuzingatia umuhimu wa mbolea, Serikali ya Awamu ya Sita imechukua hatua mbalimbali kuimarisha matumizi ya mbolea nchini. Hatua hizo ni pamoja na kuweka mazingira wezeshi kuvutia uwekezaji katika uzalishaji na biashara ya mbolea ambapo imeondoa kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa forodha kwa mitambo na mashine za kuzalisha mbolea. Vilevile baada ya kupanda kwa bei za mbolea katika soko la dunia ikiwa ni sehemu ya athari za UVIKO 19 na mgogoro wa Urusi na Ukraine, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi billioni 150 kwa ajili ya kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima katika msimu wa 2022/23 na katika msimu wa 2023/24 kiasi cha bilion 130.

Lengo la ruzuku hiyo ya mbolea ni kuwapunguzia wakulima gharama ya kununua mbolea ili kuongeza uzalishaji na tija katika Sekta ya Kilimo, kuimarisha usalama wa chakula, upatikanaji wa malighafi za viwanda na ukuaji wa uchumi.

Hatua hizo Bi. Bolle anasema zimewezesha kuongezeka kwa matumizi ya mbolea nchini kutoka tani 363,145 mwaka 2019/20 hadi kufikia tani 580,628 mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 60.

Kuongezeka kwa matumizi ya mbolea nchini kumechangia kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao kutoka tani 30,569,894 mwaka 2020/21 hadi kufikia tani 36,409,695 mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 19.

Tafiti zinaonyesha kuwa matumizi sahihi ya mbolea yanachangia takribani asilimia 20 hadi 40 ya uzalishaji wa mazao na asilimia inayobaki inachangiwa na mambo mengine ikiwemo matumizi ya mbegu bora, huduma za ugani na uzingatiaji wa kanuni bora za kilimo kwa ujumla.

Utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea unaendelea katika msimu wa 2023/24, hadi kufikia tarehe 31 Januari, 2024 matumizi ya mbolea yamefikia tani 490,858. Ni dhahiri kuwa matumizi ya mbolea yataongezeka zaidi katika msimu huu na matarajio ni kuwa uzalishaji wa mazao pia utaongezeka.



Miaka 3 ya Rais Samia Ofisini

# TFRA yatanua wigo kwa kuwavuta wawekezaji tasnia ya mbolea

## Balozi wa Urusi aahidi makubwa




*Balozi wa Urusi nchini Tanzania, Andrey Avetisyan (wa pili kutoka kulia) akiwa tayari kwa kikao baina ya wafanyabiashara wa mbolea wa Tanzania na Urusi kilichofanyika kwa njia ya mtandao katika ukumbi wa mikutano wa Kituo cha Utamaduni cha Urusi kilichopo Upanga Jijini Dar Es Salaam tarehe 15 Februari, 2024*

Na **MWANDISHI WETU**

**Kufuatia kuwepo kwa utashi** wa kisiasa na mazingira wezeshi, vitu ambavyo ni muhimu kwa dira na mwelekeo wa uchumi wa Tanzania, Mamlaka ya Udhibiti Mbolea Tanzania (TFRA) imekuwa ikifanya mikutano kadhaa na wafanyabiashara wa mbolea wa ndani na nje kuelezea fursa zilizopo katika tasnia ya mbolea.

Katikati ya Februari mwaka huu TFRA iliandaa kikao kati ya wafanyabiashara wa Tanzania na Urusi kilichofanyika Dar es Salaam.

Kikao hicho kilikuwa ni mwanzo wa kuimarisha uhusiano wa kibiashara baina ya nchi hizo mbili ili kuingiza teknolojia ya kisasa kwenye sekta ya mbolea ili kuongeza tija katika kilimo.

Katika kikao hicho mwakilishi wa TFRA. Daniel Maarifa, aliwahikikishia wafanyabiashara wa Urusi kwamba Tanzania ina malighafi za kutosha kwa ajili ya uzalishaji wa mbolea nchini.

Malighafi hizo ni pamoja na madini ya fosfeti, gesi asilia, makaa ya mawe, chokaa na madini mengine muhimu yanayopatikana sehemu mbalimbali nchini.

Balozi wa Urusi nchini Tanzania, Andrey Avetisyan, alisema kikao hicho cha Dar es Salaam kimejenga daraja imara kwa wafanyabiashara wa Urusi kushirikiana na wenzao wa Tanzania katika ujenzi wa viwanda na biashara ya mbolea

Balozi huyo alisema kwa mtazamo wake Tanzania na nchi jirani za Afrika Mashariki zina fursa lukuki kwa kuwekeza katika biashara ya mbolea.

Aliahidi kwamba ubalozi wake utaweka mkazo mkubwa katika kuimarisha uhusiano wa kibiashara kati ya Urusi na Tanzania.

Naye Afisa Uhamasishaji na Uwekezaji wa Kituo Cha Uwekezaji, Elizabeth Muzo, alitoa mwaliko kwa wafanyabiashara wa Urusi kuwekeza katika tasnia ya mbolea Tanzania kwa sababu ya kuwepo kwa soko kubwa linaloweza kuwafikia zaidi ya watu milioni 400 wa eneo hili la Afrika Mashariki na Kati.

TFRA pia ilifanya kikao na wawekezaji kutoka Falme za Kiarabu kuwaelezea fursa kadhaa zilizopo katika sekta ya mbolea kuanzia ujenzi wa viwanda, upatikanaji wa masoko, uchukuzi, malighafi, nishati, taasisi za utafiti, ujenzi wa maghala na taasisi za fedha za kutoa mikopo.



Miaka 3 ya Rais Samia Ofisini

# JUKWAA LA MIFUMO YA CHAKULA AFRIKA



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan viongozi wa Serikali na viongozi wa jukwaa la Mifumo ya chakula pamoja na washindi wawili wa Tuzo za Grand Prize, uliowashindanisha Wakulima bora kwa upande wa Vijana wa Bara la Afrika katika Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika - AGRF 2023, uliofanyika katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC), Jijini Dar es salaam tarehe 7 Septemba 2023.*

## Rais Samia afurahishwa na ongezeko matumzi ya mbolea

Na **MWANDISHI WETU**

**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan** amesema ongezeko la matumizi ya mbolea katika kilimo ni ishara kubwa kwamba sekta hiyo sasa inaleta tija kwa wakulima.

Amesema kuongezeka kwa uzalishaji kwenye miradi mbalimbali ya kilimo inayosimamiwa na vijana kupitia mradi wa Kuijenga Kesho iliyo Bora (BBT) chini ya Wizara ya Kilimo ni kipimo cha matumizi mazuri ya mbolea.

Dkt Samia alieleza hayo tarehe Agosti 7, 2023, alipokuwa akizungumza na vijana barani Afrika kuhusu jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali mbalimbali katika kuhakikisha vijana wanaingia kwenye shughuli za uzalishaji na kupunguza changamoto inayowakabili ya kukosa ajira.

Alisema ishara nyingine ni kuongezeka kwa mchango utokanao na kilimo kwenye uchumi wa nchi, kiasi cha mazao yanayopelekwa sokoni pamoja na kushuka kwa gharama za chakula sokoni.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa katika mjadala maalum wa vijana wakati wa Mkutano wa Mifumo ya Chakula Afrika uliofanyika kwenye Ukumbi wa Selous katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere Septemba 7, 2023.*

Mjadala huu ni miongoni mwa mijadala mbalimbali iliyofanyika kuanzia Agosti 5 - 8, 2023, wakati wa mkutano wa Kimataifa wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika ambapo zaidi ya washiriki 4,000 kutoka nchi mbalimbali Afrika walishiriki mkutano huo.

Kwa upande wake, Rais wa Kenya, Dkt. William Ruto, akizungumza katika mkutano huo alisema pamoja na kuwekeza katika teknolojia za kilimo cha kisasa, matumizi sahihi ya mbolea na mbegu husaidia katika kuongeza kipato na kuleta mapinduzi ya kilimo barani Afrika.

Alisema nchi yake inawasaidia wakulima kuongeza uzalishaji wa chakula kwa kuwawezesha kupata mbolea na mbegu kwa bei nafuu.

Kwa mwaka 2023 Kenya ilisajili wakulima 5,000 na kusambaza mbolea kwa kutumia mtandao wa kielektroniki ili kuondoa madalali na matapeli ambao mara zote huwafanya wakulima kupata mbolea kwa gharama kubwa.

Kenya imepunguza gharama ya mbolea kutoka dola 50 hadi dola 20 kwa tani moja. Kupitia kampuni ya mbolea ya YARA Kenya imeongeza kiwango cha utoaji wa mbolea msimu uliopia na hivyo kutegemea kuvuna magunia milioni 44 hadi milioni 61 ya mahindi kutokana na kutumia mbegu bora na kuhakikisha upatikanaji mzuri wa mbolea utakaochochea kupatikana kwa mazao mengi shambani.

Mkutano huo ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwemo Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango na viongozi mbalimbali wa ngazi za juu kitaifa.



## Miaka 3 ya Rais Samia Ofisini

# Rais Samia ana mchango mkubwa uanzishwaji wa kiwanda cha mbolea ITRACOM

## Kiwanda kuzalisha tani 1,000,000 ifikapo Juni 2024

Na **MWANDISHI WETU**

**ITRACOM Fertilizers Limited (IFL)** ni Kampuni iliyosajiliwa nchini Tanzania kuzalisha mbolea ya mseto wa mbolea za chumvi chumvi na mbolea ya asili (Organo-Mineral Fertilizers - FOMI). Kampuni hii ipo Dodoma-Tanzania katika eneo la viwanda la Nala ambako imeanzisha kiwanda chake.

Mkurugenzi Mkuu wa IFL Nduwimana Nazaire anasema ujio wa kiwanda hiki unatokana na juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dk Samia Suluhu Hassan, wakati akiwa bado ni Makamu wa Rais wa Awamu ya Tano katika jitihada za kupambana na upungufu wa mbolea uliojitikeza wakati huo.

Katika ziara yake aliyoifanya nchini Burundi Mhe. Rais Samia alibaini kuwa kuna uzalishaji wa mbolea nchini humo hivyo aliomba uwezekano wa uwekezaji huu wa kimkakati ufanyike pia Tanzania. Mwekezaji huyo wa Burundi aliitikia mwaliko huo na mnamo mwaka 2020 mchakato wa uwekezaji ulianza na Julai 2021 ujenzi wa kiwanda ulianza rasmi. Ujenzi wa kiwanda hicho ulikwenda kwa kasi isiyokuwa ya kawaida kutokana na mazingira wezeshi ya serikali ya Awamu ya Sita ambapo ilipofika Desemba 2022 uzalishaji ulianza kwa kutumia mtambo wa kwanza uliokuwa tayari umesimikwa.

Nduwimana anasema ITRACOM inazalisha mbolea za mseto wa chumvi chumvi na mbolea ya asili, hivyo kuzifanya mbolea hizo kuitwa FOMI (yaani Organo-Mineral Fertilizers). Kwa mujibu wa Nduwimana, mbolea za FOMI ni mchanganyiko wa mbolea za chumvi chumvi (Urea, Diammonium Phosphate (DAP), Muriate of Potash (MoP)); na mbolea za asili ni pamoja na samadi, mwamba wa fosfeti na chokaa Kilimo).

Mkurugenzi Mkuu huyo anasema IFL inazalisha mbolea za aina tatu kwa sasa hivi ambazo ni

FOMI OTESHA ambayo ni mbolea ya kupandia yenye virutubisho vitano muhimu [Fosforasi (22%), Nitrojeni (9%), Potasiamu (4%), Kalsiamu (13%) na Magnesiamu (2%). Mbolea hii inafaa kwa kupanda mazao ya chakula na mboga.

Aina nyingine inayozalishwa na Itracom inaitwa FOMI KUZIA ni mbolea ya kukuzia yenye virutubisho vinne muhimu [Nitrojeni (21%), Potasiamu (8%), Kalsiamu (4%) na Magnesiamu (2%). Mbolea hii inafaa zaidi kwa mazao ya chakula, mboga mboga, na hasa mazao ya nafaka.

Mbolea ya FOMI NENEPESHA Nduwimana anasema ni mbolea ya kukuzia, hasa hutumika kwenye mazao ya mizizi kama viazi vitamu na mviringo, mihogo, karoti, vitunguu n.k. Mbolea hii ina virutubisho vinne [Nitrojeni (11%), Potasiamu (22%). , Kalsiumu (4%) na Magnesiamu (2%)].

Nduwimana anafafanua kuwa faida kuu ya uwekaji mbolea za FOMI ni kuongeza mavuno ya mazao na kuboresha afya ya udongo. Mbolea za FOMI anasema husaidia kurejesha afya ya udongo katika nyanja tatu ikiwemo afya ya udongo ya kemikali (Chemical Soil Health) kupitia mchanganyiko wake wa virutubisho unaoongeza hifadhi ya virutubisho vya udongo na hivyo rutuba na afya ya udongo kifizikia (Physical Soil Health) kupitia sehemu yake ya kikaboni (mboji) inayojenga muundo wa udongo kwa ajili ya uingizaji hewa bora wa udongo na mtiririko wa maji.

Nyanja au njia ya tatu ya kurejesha afya ya udongo ni ya Kibaiolojia (Biological Soil Health) kupitia sehemu yake ya kikaboni (Mboji) ambayo hutumika kama chakula cha wadudu na viumbe rafiki vilivyomo kwenye udongo ambavyo husaidia kuozesha mabaki ya viumbe hai ikiwamo mimea na wanyama.

'Kwa hiyo, kauli mbiu yetu ni "Ongeza Mavuno ya Mazao, Boresha hali ya udongo kwa kutumia Mbolea ya FOMI" anasema Nduwimana.

Kwa upande wake Naibu Mkurugenzi Mkuu wa IFL Dkt.Kenneth Masuki anasema

kwa sasa IFL inaendesha mitambo miwili ya kuzalisha mbolea yenye uwezo wa kuzalisha tani laki Mbili (200,000) kila mmoja na kufikia Juni 2024, IFL inatarajiwa kukamilisha uwekazaji wa mitambo yote iliyopangwa, yenye uwezo wa kuzalisha tani Milioni Moja (1,000,000) za mbolea ya FOMI kwa mwaka.

Dkt. Masuki anaongeza kuwa kutakuwa na kiwanda cha chokaa cha kilimo chenye uwezo wa kuzalisha tani 200,000. Vilevile kuna kiwanda cha kuchakata madini ya Fosfeti kilichopo Manyara chenye uwezo wa kuzalisha tani laki Mbili (200,000) za fosfeti inayotumika kama malighafi ya uzalishaji wa mbolea.


Kwa mujibu wa Dkt Masuki mbolea zinazozalishwa hasa "FOMI Otesha", "FOMI Kuzia" na "FOMI Nenepesha" tayari ziko sokoni na wakulima ambao tayari wameshuhudia ufanisi wake baada ya kuzitumia, anaongeza kuwa mbolea hizi zimefika kwenye zaidi ya mikoa 23 ya Tanzania Bara.

Dkt. Masuki anaeleza kuwa mbolea za FOMI zikiwa mpya katika soko la Afrika, uzalishaji wake unaiweka IFL kama mojawapo ya wachangiaji wakuu wa ajenda ya AFSF 2023 ambayo inalenga kuiweka Afrika kama mahali pa uvumbuzi, uwekezaji na kuendeleza mfumo wa chakula wenye nguvu zaidi wa aina mbalimbali na ustahimilivu.



## Miaka 3 ya Rais Samia Ofisini

# Namna mfumo wa kidijitali wa mbolea za ruzuku unavyodhibiti vitendo vya ubadhirifu



FUNCTIONALITY

The DIGITAL FERTLIZER SUBSIDY DISTRIBUTION AND PAYMENT System offers various features to streamline your tasks and improve efficiency.

DISTRIBUTION NETWORK

In this module you are able to register all your distribution networks from Branches, Warehouses and Agro-dealers in your network.

BRANCHES

Here you will be able to see a list of all your registered Branches. You can also be able to register a new branch

ADD NEW BRANCHES

1. Go to Distribution Network>Branches
2. On the right-hand side of the page there is a + sign which signifies Add/Register new branch
3. Click that sign to open a new registration form for your branches

Na **MWANDISHI WETU**

**Baada ya Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan** kuamua kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima kutokana na bei ya bidhaa hiyo kupanda mwanzoni mwa mwaka 2019/2021. Serikali kupitia Waziri wa Kilimo Hussien Bashe ilikuja na maono ya kubadilisha namna ya utoaji wa mbolea za ruzuku kwa wakulima.

Katika maono yake Waziri Bashe alitaka kuanza kwa kubaini mkulima ni nani?. Na katika kujibu wazo hili ikaamuliwa kuwa na mfumo maalumu utakaomsajili mkulima, ukubwa wa shamba lake, mfanyabiashara na wakala wa mbolea pamoja na kubainisha aina za mbolea na bei zake.

"Ili kuhakikisha mbolea za ruzuku zinawafikia walegwa, ni lazima tuwatambue, wajisajili, wasajili ukubwa wa mashamba yao na aina ya mazao wanayoyalima ili itusaidie kutoa mbolea kulingana na mahitaji ya zao na ukubwa wa shamba la mkulima" Alisisitiza Waziri Bashe alipokuwa akizindua mfumo wa kidijitali wa mbolea za ruzuku jijini Dodoma.

Akiwasilisha makadirio ya bajeti kwa mwaka 2023/2024, Waziri Bashe alisema kwa mara ya kwanza katika historia Tanzania imeweza kuwatambua wakulima wa Tanzania kwa majina yao kamili, mahala walipo, ukubwa wa mashamba na maeneo wanayofanyia shughuli zao za kilimo.

Pia, Waziri anaeleza nia ya serikali kupitia Mamlaka kuendelea kusajili wakulima na kutoa kadi maalum ya kuwatambua huku lengo likiwa ni kusajili wakulima 7,000,000 ifikapo mwaka 2025.

Meneja wa TEHAMA na Takwimu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Robert Mtendamema anasema, Mamlaka imepewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea unaofanyika kwa mfumo wa kidigitali ili kubaini aina zote za ubadhirifu zinazofanyika pamoja na kuondoa udanganyifu uliojitokeza kwenye utekelezaji wa ruzuku za miaka ya nyuma.

Kufuatia mwenendo wa utekelezaji wa mpango huo, mwishoni mwa mwezi Desemba, 2023 wafanyabiashara na wakulima wasiokuwa waaminifu wa Mkoa wa Songwe walibainika wakinunua

Inaendelea Uk > 17



## Miaka 3 ya Rais Samia Ofisini

< Inatokaa Uk 16

# Namna mfumo wa kidijitali wa mbolea za ruzuku unavyodhibiti vitendo vya ubadhirifu

kiasi kikubwa cha mbolea na hivyo kuifanya Mamlaka kwa kushirikiana na mkoa husika kufanya uchunguzi ambapo watuhumiwa wapatao watatu walifikishwa mahakamani.

Akizungumza hivi karibuni, Louis Kasera Mwenyekiti wa Kamati ya Ruzuku kitaifa anaeleza kuwa mfumo wa kidijitali haudanganyi na kwamba kwa namna ulivyoundwa unatunza kumbukumbu za kila kitu kinachofanyika ndani ya mfumo huo.

Kasera anasema Mamlaka imejipanga vizuri katika kuhakikisha kuwa inawashughulika watu wote wanaofanya ubadhirifu kwa kuwachukulia hatua kali za kisheria.

"Tungependa jamii ijue kuwa hakuna ujanja mbele ya mfumo wa kidijitali kwani unachukua taarifa za kila mtu anayeingia kwenye mfumo na kama utafanya udanganyifu wowote tutakukamata tu" anasema Kasera. Uchunguzi wa kina uliofanyika Mkoani Songwe uliwabaini watuhumiwa watatu wa mbolea za ruzuku waliocheza na mfumo wa mbolea za ruzuku.

Wakili wa Serikali katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Songwe, Joseph Mwakasege anaeleza makosa wanayokabiliana watuhumiwa hao kuwa ni pamoja na kosa la kuhujumu Uchumi kosa lisilokuwa na dhamana.



*Louis Kasera, Mwenyekiti wa Kamati ya Ruzuku Taifa*

Anaeleza makosa mengine yanayowakabili watuhumiwa hao ni kuendesha genge la uhalifu kwa kuingilia mfumo wa mbolea za ruzuku na kuisababishia serikali hasara ya takribani Shilingi bilioni 1.422 kujipatia mifuko 205 ya mbolea kinyume na utaratibu, kukwepa kodi ipatayo Shilingi milioni 129 iliyopaswa kulipwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mkoani Songwe, kushindwa kutoa risiti za kielektronic zinazokubalika na TRA,

Watuhumiwa hao pia wameshtakiwa kwa makosa ya mtandao kwa kuingilia mfumo wa mbolea za ruzuku, kucheza na laini za wakulima kwa kuiba namba za siri na kujipatia mbolea walizoziuza nje ya mfumo kinyume na utaratibu na kosa la kutakatisha fedha.

Wakili Mwakasege anahitimisha kwa kusema, kutokana na ubadhirifu huo wakulima waliostahili kununua mbolea kwa kupitia mfumo wa ruzuku hawakuweza kupata huduma kwani namba zao za siri zilikuwa zimekwisha tumika na hivyo kuwasababishia usumbufu kinyume na lengo la serikali la kutaka kuwapunguzia mzigo wa gharama wakulima.



*Mkulima Rizika Bolgias Ngonyani wa Madaba Mkoani Ruvuma akitoka kwa wakala wa mbolea za ruzuku mara baada ya kunuua mifuko 3 ya mbolea aina ya SA kutoka kwa wakala Mtewele General raderss and Insurance Agent ya mjini Njombe.*



Miaka 3 ya Rais Samia Ofisini



*Mwonekano wa kiwanda cha mbolea cha Itracom chenye uwezo wa kuzalisha kiasi cha tani milioni moja ya mbolea ya asili itakayopunguza utegemezi wa mbolea kutoka nje ya nchi kwa kiasi kikubwa mara baada ya uzalishaji wake kukamilika.*

# Tanzania yazoa sifa kuandaa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika

Na **MWANDISHI WETU**

**Ushiriki wa Rais Samia Suluhu Hassan** kwa kuwa mstari wa mbele katika duru za majadiliano ya masuala ya kilimo kimataifa ulifanikisha Tanzania kuwa mshindi wa kuandaa Jukwaa la Mifumo ya Chakula barani Afrika Septemba mwaka jana.

Jukwaa hilo lililofanyika katika Ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam kuanzia Septemba 5 hadi 8 lilihudhuriwa na wadau wa maendeleo kutoka taasisi mbalimbali za kimataifa.

Taasisi hizo ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo Afrika, Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo (FAO) na Shirika la Mifumo ya Chakula Barani Afrika (AGRA).

Jukwaa hilo, ambalo lilihudhuriwa na zaidi ya washiriki 3,000, lilikuwa ni fursa kubwa kwa Tanzania kuvutia uwekezaji katika nyanja mbalimbali ikiwemo sekta ya kilimo na biashara.

Washiriki hao walijadili, pamoja na mambo mengine, umuhimu wa kilimo endelevu na kinachozingatia hifadhi ya mazingira na kinachohimili mabadiliko ya tabianchi na masuala ya utafiti.

Akihutubia jukwaa hilo, Rais Samia aliwaambia washiriki -- wanasayansi na watafiti – kwamba serikali yake imeweka mikakati ya kuhakikisha kwamba sekta ya kilimo inachangia asilimia 10 kwenye pato la taifa ifikapo 2030.

Alisema katika kutekeleza azma hiyo, serikali imewekeza katika kushirikisha vijana na wanawake katika biashara za kilimo kwa kutenga shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kutoa mikopo.

Washiriki wa jukwaa hilo walitilia mkazo suala la upatikanaji wa uhakika wa chakula barani Afrika ili kulisha ongezeko kubwa la idadi ya watu kwa miaka ijayo.

Maazimio muhimu ya majadiliano la jukwaa hilo yalijikita zaidi kwenye msukumo wa uwekezaji katika sekta ya kilimo kwa mustakabali wa usalama wa chakula kuelekea 2030.



## Miaka 3 ya Rais Samia Ofisini



*Mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Anthony Diallo akiwa na baadhi ya Wajumbe wa Bodi hiyo akizungumza wakati wa kikao kifupi na uongozi wa Mpaka wa Tunduma na Malawi kilicholenga kujadili namna nzuri ya kuongeza udhibiti wa utoroshwaji wa mbolea unaofanyika mipakani pamoja na kusikiliza changamoto wanazokutana nazo wakati wa kukagua bidhaa za mbolea zinazopita bandarini hapo kwenda nchi jirani tarehe 17 Oktoba, 2023.*

# Ijue sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania

Na **MWANDISHI WETU**

### Utangulizi

**Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA)** ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Kilimo iliyoanzishwa kwa Sheria Na. 9 ya Mwaka, 2009. Mamlaka ilianza kutekeleza majukumu yake Agosti, 2012. Jukumu kuu la Mamlaka ni kudhibiti ubora wa mbolea kwa kusimamia biashara ya mbolea katika mnyororo wa thamani ikiwemo utengenezaji, uingizaji nchini, usafirishaji nje ya nchi, uuzaji na matumizi ya mbolea kwa ajili ya kilimo kwa lengo la kuhakikisha mbolea inayomfikia mkulima ina ubora unaokidhi viwango.

### Majukumu

Mamlaka katika kutekeleza majukumu yake inaongozwa na Sheria ya mbolea. Sheria ya mbolea ambayo inaweka masharti ya utengenezaji, uingizaji nchini, usafirishaji nje ya nchi, uuzaji na matumizi ya mbolea kwa ajili ya kilimo. Aidha, kifungu cha 4(1) cha Sheria kimeainisha majukumu mahususi ambayo kwa ujumla wake yanafanikisha utekelezaji wa jukumu kuu ambalo ni udhibiti ubora wa mbolea.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 4(1) Mamlaka itakuwa chombo cha udhibiti katika tasnia ya





mbolea na kipekee-

(a) itadhibiti masuala yote yanayohusiana na ubora wa mbolea, visaidizi vya mbolea na mitambo ya utakasaji;

(b) itasajili wafanyabiashara wote wa mbolea na visaidizi vya mbolea na maeneo yao;

(c) itatoa leseni kwa wafanyabiashara wa mbolea;

(d) itatoa vibali kwa ajili ya mbolea na visaidizi vya mbolea kuingizwa nchini na kusafirishwa nje ya nchi;

(e) itatunza rejesta ya mbolea na visaidizi vya mbolea, mitambo ya utakasaji na viwanda vya kutengeza mbolea;

(f) itatunza na kutangaza mara kwa mara rejesta ya wafanyabiashara wa mbolea;

(g) itatekeleza mikataba ya kimataifa iliyoridhiwa kuhusiana na mbolea;

(h) itadhibiti na kusimamia uingizaji nchini, uzalishaji, usafirishaji nje ya nchi, ushughulikiaji, uhifadhi, na uteketezaji wa mbolea au visaidizi vya mbolea;

(i) itakusanya, kutunza na kuchapisha taarifa zinazohusiana na mbolea na kisaidizi cha mbolea;

(j) itaandaa miongozo juu ya usimamizi sahihi na udhibiti wenye ufanisi wa mbolea na visaidizi vya mbolea;

(k) kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa, itafanya makongamano ya kutoa elimu kwa umma juu ya matumizi sahihi na usimamizi wa mbolea na visaidizi vya mbolea;

(l) itatoa mafunzo ya mara kwa mara kwa wadau kuhusu masuala ya mbolea;

(m) itasajili wakaguzi na wachambuzi;

(n) itakagua au kuwezesha ukaguzi wa mbolea au visaidizi vya mbolea kwa ajili ya kujihakikishia ubora;

(o) itatekeleza sera, mikakati na mipango inayohusiana na maendeleo ya tasnia ya mbolea;

(p) itatoa ushauri wa kitaalamu kwa Serikali na taasisi zingine katika masuala yote yanayohusiana na usimamizi na udhibiti wa mbolea na visaidizi vya mbolea;

(q) itafanya au kuwezesha kufanyika utafiti kuhusiana na mbolea na visaidizi vya mbolea;

(r) itakuza ushirikiano kati ya taasisi na taasisi nyingine au mashirika na wadau;

(s) itashirikiana na mashirika ya kitaifa na kimataifa kwenye masuala yote yanayohusiana na mbolea na kisaidizi cha mbolea;

(t) itatekeleza maelekezo maalum na ya ujumla ya Mamlaka;

(u) itadhibiti bei ya mbolea kwa kuzingatia njia sahihi kama zitakavyoainishwa katika kanuni;

(v) itaainisha njia au mfumo sahihi wa uingizaji nchini na usafirishaji nje ya nchi wa mbolea au visaidizi vya mbolea;

(w) itatekeleza majukumu mengine yoyote kama inavyoweza kupewa katika utekelezaji wa majukumu chini ya Sheria hii; na

(x) itahakikisha kwamba inazingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.



# Asante Rais Samia kwa MAELEKEZO

**#KAZI IENDELEE**

*Jarida hili hutolewa na:*
***Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA)***
*Mtaa wa Kilimo, Jengo la Kilimo I Complex,*
*Barabara ya Mandela, S.L.P. 46238 Dar es Salaam.*
*Simu. +255 22 2861939*
*Baruapepe: info@tfra.go.tz*
*Tovuti: www.tfra.go.tz*